# Mafunzo ya kushughulikia kisa:
# Mwongozo wa Mwendeshaji

## 1. Malengo

Kufikia mwishoni mwa mafunzo Washiriki wataweza:

- Kueleza jinsi ya kuchukua mbinu inayomlenga mnusurika katika kushughulikia wasiwasi au malalamiko kuhusu kulinda usalama.
- Kuonyesha umuhimu wa idhini na faragha.
- Kutumia mchakato wa kushughulikia kisa katika kuitikia wasiwasi au malalamiko kuhusu kulinda usalama.

## 2. Maandalizi ya washiriki

Washirika wanasoma:

- Kupokea na kuitikia ripoti ya dhuluma ya kingono, unyonyaji au unyanyasajiwa kingono (SEAH) nchini Nigeria
- Idhini na faragha nchini Nigeria
- Kushughulikia kisa kwa Mashirika ya Kijamii nchini Nigeria
- Slaidi za mafunzo ya kushughulikia kisa

# 3. Ajenda

Mafunzo ya mtandaoni yatachukua saa 3.5 (ikijumuisha muda wa mapumziko). Inapendekezwa kuwa hii igawanywe katika vipindi viwili vifupi vilivyo na angalau mapumziko ya nusu saa ili kutumia vyema nafasi ya kujifunza kupitia kwenye mtandao.

Kwa mafunzo ya ana kwa ana, nyakati zinaweza kubadilishwa ili kuruhusu mafunzo kufanyika kwa muda mfupi zaidi ikiwa inapendelewa.

Ajenda ya mafunzo

| Muda | Shughuli |
|---|---|
| **Dakika 30** | A. Kukaribisha na utambulisho |
| **Dakika 40** | B. Kuitikia ripoti, idhini na faragha |
| **Dakika 20** | C. Kushughulikia kisa kwa Mashirika ya Kijamii |
| **Dakika 30** | Mapumziko |
| **Dakika 30** | D. Kazi ya kikundi- Kushughulikia kisa |
| **Dakika 45** | E. Wasilisho- Kushughulikia kisa |
| **Dakika 15** | F. Kufunga na kupiga kura |

# A. Utambulisho

| Muda | Shughuli | Slaidi/ Rasilimali | Teknolojia |
|---|---|---|---|
| Dakika 30 | Nafasi ya kujadili kwa mzunguko | 1-5 | Hakuna |
| **Matokeo ya Mafunzo** | Kutambulisha washiriki wao kwa wao. Kujadili malengo ya mafunzo.<br>Kanuni za msingi zilizokubaliwa. | | |
| **Shughuli** | **Kukaribisha**<br>Kukaribisha kila mtu kwenye mafunzo.<br>**Utambulisho**<br>Shiriki jina lako na Shirika lako la Kijamii.<br>**Malengo**<br>Wasilisha malengo ya mafunzo.<br>**Kukubali kuhusu kanuni za msingi**<br>Kumbuka kuhusu kiungo cha faragha kwa mfumo wa kulinda usalama.<br>**Uzoefu**<br>Tumia aikoni ya kidole gumba kuonyesha ikiwa umeitikia kisa au wasiwasi wa kulinda usalama hapo awali.<br>Washiriki wa mafunzo ya ana kwa ana wanaweza kuinua mikono yao ikiwa wameitikia kisa au wasiwasi wa kulinda usalama hapo awali. | | |

# B. Kuitikia ripoti, idhini na faragha

| Muda | Shughuli | Slaidi/ Rasilimali | Teknolojia |
|---|---|---|---|
| Dakika 40 | Kuchemsha ubongo, kuwasilisha na kazi ya vikundi | 6-17<br>Kupokea na kuitikia<br>ripoti ya dhuluma wa kingono, unyonyaji au unyanyasaji wa kingono (SEAH) nchini Nigeria<br>Idhini na faragha nchini Nigeria | Slaidi<br>Vikundi vidogo |

| | |
|---|---|
| **Matokeo ya Mafunzo** | Washirika washiriki wanaweza kueleza mbinu inayomlenga mnusurika. Washirika washiriki wanaweza kueleza jinsi ya kuitikia ripoti.<br>Washirika washirikiwanaweza kueleza wajibu wa kuwatunza washukiwa wa uhalifu, idhini na faragha. |

| | |
|---|---|
| **Shughuli** | **Kuchemsha ubongo na kuwasilisha- dakika 15**<br>Kutoka kwa Kupokea na kuitikia ripoti ya dhuluma ya kingono, unyonyaji na unyanyasaji wa kingono (SEAH) nchini Nigeria<br>Slaidi ya 6- Andika kwenye slaidi hii ni nini maana ya mbinu inayomlenga mnusurika. Mwendeshaji anaweza kuandika maelezo kwenye slaidi.<br>Ana kwa ana- Mwendeshaji anaweza kumwalika mshiriki kuandika majibu kwenye chati mgeuzo.<br>Slaidi ya 7- Kagua mchoro wa mbinu inayomlenga mnusurika.<br>Slaidi ya 8-9- Kagua, Angalia, Sikiliza na Uunganishe kanuni zilizochukuliwa kutoka mbinu za Msaada wa Kwanza wa Kisaikolojia.<br>Slaidi ya 10- Andika kwenye slaidi hii jinsi tunapaswa kuitikia ripoti. Mwendeshaji anaweza kuandika maelezo kwenye slaidi.<br>Ana kwa ana- Mwendeshaji anaweza kumwalika mshiriki kuandika majibu kwenye chati mgeuzo.<br>Slaidi ya 11- Kagua Mambo ya Kufanya na Kutofanya unapoitikia ripoti.<br>**Kazi ya kikundi - dakika 10**<br>Gawa washiriki katika vikundi 3.<br>Gawia kila kikundi slaidi moja na swali. Kila kikundi kitaandika majibu ya maswali yao katika slaidi za Google. |

Ana kwa ana- Washiriki waandike majibu kwenye chati mgeuzo na swali kuandikwa juu ya ukurasa.

- Kikundi cha 1- Je, wajibu wetu kwa mshukiwa wa uhalifu ni upi?

Kutoka kwa Kupokea na kuitikia ripoti ya dhuluma ya kingono, unyonyaji au unyanyasaji wa kingono (SEAH) nchini Nigeria

- Kikundi cha 2- Ni wakati upi tunahitaji idhini iliyoarifiwa?
- Kikundi cha 3- Je, faragha ina maana

gani? Kutoka kwa Idhini na faragha nchini Nigeria**Mawasilisho kutoka kwa vikundi**

**dakika 10**

Mwendeshaji anaweza kuimarisha maudhui na slaidi husika (13, 15 na 17 mtawalia) ikihitajika.

## C. Kushughulikia kisa kwa Mashirika ya Kijamii

| Muda | Shughuli | Slaidi/ Rasilimali | Teknolojia |
|---|---|---|---|
| Dakika 20 | Mawasilisho | 18-21<br>Kushughulikia kisa kwa Mashirika ya Kijamii nchini Nigeria | Slaidi |
| **Matokeo ya Mafunzo** | Washiriki wamekagua mchakato wa kushughulikia kisa | | |
| **Shughuli** | **Mawasilisho**<br>Wasilisha slaidi na ujibu maswali. | | |

Mapumziko

# D. Kazi ya kikundi- Kushughulikia kisa

| Muda | Shughuli | Slaidi/ Rasilimali | Teknolojia |
|---|---|---|---|
| Dakika 30 | Kazi ya kikundi | 22-26 | Slaidi za Google za Vikundi vidogo |
| **Matokeo ya Mafunzo** | Washiriki wametumia mfano wa kisa ili kuonyesha jinsi wangeitikia kisa kilichoripotiwa. | | |
| **Shughuli** | Wasilisha mfano wa kisa: | | |

*Unatembelea mradi wako katika jamii. Mwanajamii anakuja kukuambia kuwa mmoja wa wafanyakazi wako ana uhusiano na msichana wa miaka 14 katika jamii. Inadaiwa kuwa uhusiano huu umekuwa ukiendelea kwa muda wa miezi 6, na kuwa mfanyakazi huyo anafanya ngono na msichana huyo.*

*Familia ya msichana huyo inafahamu kuhusu uhusiano huo lakini hakuna mmoja wao ameripoti mfanyakazi huyo kwa shirika, inaonekana hii ni kwa sababu uhusiano huo unawapa usaidizi wa kifedha – inadaiwa kuwa mfanyakazi huyu anamlipia msichana huyo gharama za shule, kumnunulia zawadi na kadhalika.*

*Suala hilo lilijitokeza wakati mama ya msichana huyo alimueleza rafiki yake kuhusu uhusiano huo, naye rafiki huyo aliyekasirishwa na jambo hilo akaamua kukueleza.*

Maswali:

- Je, unahitaji kufanya nini na habari uliyopewa? Je, ungemwambia nani? Je, ungewaambia nini?
- Je, unawezaje kusaidia au kumhakikishia mtu anayefichua dhuluma hiyo?
- Je, ungetarajia nini kifanyike baada ya kuripoti habari hiyo?

Gawa washiriki katika vikundi 4 vilivyochanganyika. Vikundi viwili vitaitikia kana kwamba wao ndio waratibu wa kulinda usalama na vikundi viwili vitaitikia kana kwamba ni wafanyikazi wasio na jukumu maalum la kulinda usalama.

Kipatie kila kikundi seti ya slaidi na uwaalike kujibu maswali.

Washiriki wanafanya kazi katika vikundi vyao kwa kutumia slaidi za Google ili kusaidia mawasilisho ya baadaye.

Ana kwa ana- Onyesha mfano wa kisa na maswali. Washiriki waandike majibu kwenye chati mgeuzo.

Waendeshaji wasaidie panapohitajika.

# F. Mawasilisho ya kazi ya vikundi

| **Muda** | **Shughuli** | **Slaidi/ Rasilimali** | **Teknolojia** |
|---|---|---|---|
| Dakika 45 | Mkutano Mkuu | 22-26 | Slaidi za Google |
| **Matokeo ya Mafunzo** | Washiriki wametumia mfano wa kisa ili kuonyesha jinsi wangeitikia kisa kilichoripotiwa. | | |
| **Shughuli** | Kila kikundi kinawasilisha mijadala ya kikundi chao. | | |

Ruhusu mawasilisho ya dakika 5 na majadiliano ya dakika 5 kwa kila kikundi.

Mwendeshaji anaunganisha mambo muhimu.

# G. Kufungwa kwa mafunzo

| Muda | Shughuli | Slaidi/ Rasilimali | Teknolojia |
|---|---|---|---|
| Dakika 15 | Tafakari ya mtu binafsi | 27 | Kura ya maoni kupiga kura |

**Matokeo ya Mafunzo** Washiriki wametafakari kuhusu mafunzo yao

**Shughuli**

Kila mshiriki anatumia *neno/kifungu 1 cha maneno* kutaja mafunzo waliyopata kuwa muhimu zaidi kutoka kwenye mafunzo hayo.

Waalike Washiriki wakamilishe kwa **kupiga kura:**

**Kupiga kura**:

1. Nina ufahamu wazi wa jinsi ya kushughulikia kisa- Ndio, Kiasi, La
2. Nina uhakika kuwa ninaweza kushughulikia kisa katika shirika ninaloshauri- Ndiyo, Kiasi, La
3. Uendeshaji ulikuwa- Mzuri sana, Sawa, duni
4. Mbinu za mafunzo zilikuwa- Nzuri sana, Sawa, duni

Ana kwa ana- Andika maswali haya manne kwenye chati mgeuzo na uwaulize washiriki kuweka alama kwa majibu yao.

| | Ndiyo | La | Kiasi |
|---|---|---|---|
| Nina ufahamu wazi wa jinsi ya kushughulikia kisa | | | |
| Nina uhakika kuwa ninaweza kushughulikia kisa katika shirika ninaloshauri | | | |

| | Nzuri sana | Sawa | Duni |
|---|---|---|---|
| Uendeshaji ulikuwa | | | |
| Mbinu za mafunzo zilikuwa | | | |

Waendeshaji wanashukuru washiriki wote kwa ushiriki wao.



RESOURCE & SUPPORT HUB

UKaid from the British people

# Marejeleo

- Kushughulikia kisa kwa Mashirika ya Kijamii nchini Nigeria
- Idhini na faragha nchini Nigeria
- Kupokea na kuitikia ripoti ya dhuluma ya kingono, unyonyaji au unyanyasajiwa kingono (SEAH) nchini Nigeria

Hati hii ni matokeo ya mradi uliofadhiliwa na shirika la UK aid kutoka kwa serikali ya Uingereza. Hata hivyo, maoni yaliyotolewa, na habari iliyo ndani yake sio lazima ziwe zile za au zilizoidhinishwa na serikali ya Uingereza, ambao hawawezi kukubali jukumu la maoni kama hayo au habari au kwa utegemezi wowote uliowekwa kwao.

Chapisho hili limeandaliwa kuwa mwongozo wa jumla wa kimaslahi tu, na haujumuishi ushauri wa kitaalam. Habari iliyomo kwenye chapisho hili haipaswi kufanyiwa kazi bila kupata ushauri maalum wa wataalamu. Hakuna uwakilishi au dhamana (inayoelezea au iliyodokezwa) inayotolewa kuhusu usahihi au ukamilifu wa habari iliyo kwenye chapisho hili, na, kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria, hakuna shirika au mtu yeyote anayehusika katika kutengeneza hati hii anayekubali au kuchukua dhima yoyote, jukumu au wajibu wa utunzaji wa matokeo yoyote ya mtu yeyote anayechukua hatua, au anayekataa kuchukua hatua, kwa kutegemea habari iliyo kwenye chapisho hili au uamuzi wowote unaoitegemea.



RESOURCE & SUPPORT HUB

UKaid from the British people